# KCPE ASSESSMENT ONE

STEP FLYER

## DARASA LA NANE

## JARIBIO LA KWANZA - 2020

# 8

**Muda: Saa 1 Dak 40**

# KISWAHILI LUGHA

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.

2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.

3. Ukisha chagua jibu lolote lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.

5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:
   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu zako wewe mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.

7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.

8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.

9. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ni sahihi. Chagua jibu hilo.

10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

*Mfano*

**21.** Kamilisha methali: Ukiona vyaelea_________

A. vyaenda  B. vyaundwa
C. vyazima  D. vyaisha

Jibu sahihi ni B

**Katika karatasi ya majibu**

**11** [A] [B] [C] [D]  **21** [A] ~~[B]~~ [C] [D]  **31** [A] [B] [C] [D]  **41** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali 21, kisanduku chenye herufi B ndicho kilochochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Karatasi hii ya maswali ina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

***Soma vivungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Juma Suleiman Mapunda alipojiunga na shule ya chekechea ya Amani, walimu wake walitambua kuwa alikuwa na kipawa cha ____1____. Baada ya muhula ____2____ tu __3____ aliweza kusimama jukwaani kukariri na kughaini mashairi ya ____4____, yaani yenye mishororo mitatu katika kila ubeti; walimu na wanafunzi wenzake wakawa ndio ______5 yake. Walimu walimpa mazoezi zaidi ili ____6____. Kadhalika, Juma ____7____ masomo kiasi kwamba katika darasa la tano aliweza kutambua aina za vivumishi kama vile: _____8 , pamoja na mifano ya vokali kwa mfano, ____9____.

1. A. kigani B. kipekee C.kihalili D. kiasili
2. A. moja B. mumoja C. mmoja D. mbili
3. A. ! B. ... C. , D. ;
4. A. tathnia B. tarbia C. tathlitha D. takhmisa
5. A. halaiki B. msoa C. mashabiki D. hadhira
6. A. aimarike B. waimarishe C. aimarishe D. waimarike
7. A. aliuthamini B. alizithamini C. aliyathamini D. aliithamini
8. A. kijanja, tano, langu, leo B. sana, nane, fupi, kama
   C. nyingine, ajabu, mwenyewe, kisha D. kadha, yule, chungu, lote
9. A. a, b, ch B a, e, i C.a, dh, e D. a, ch, o

Ukiwatembelea watoto katika wadi ___10___ hospitalini msimu wa masika utagundua _11____ wao watakuwa wakiuguza ____12____ za kuepukika. Wale walioachwa vifua wazi wakati wa baridi watakuwa wakiugua ____13____ huku ____14____ ovyo.

Aidha kwingineko watu wazima wanaweza kubanwa na ___15___ ambao ni ugonjwa wa mapafu unasababishwa na bakteria wanaodhoofisha mfumo wa upumuaji.

10. A. yote B. zozote C. wowote D. yeyote
11. A. baadhi B. wengine C. wengi D. kati ya
12. A. uwele B. mawenge C. mawele D. ndwele
13. A. ukambi B. kifaduro C. malaria D. homa
14. A. wakijikohoza B. wakijikohohea C. wakijiholea D. wakikohoswa
15. A. mkamba B. mafua C. kifuakikuu D. kikohozi

***Kuanzia nambari 16 mpaka 30, jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.***

**16.** Ni herufi ipi ambayo haipatikani katika herufi za alfabeti za Kiswahili?

A. ng B. ng'
C. ny D. n

**17.** Eleza viambishi **ji** vimetumikaje katika sentensi hii?

**Mkimbia<u>ji</u> ame<u>ji</u>shindia <u>ji</u>kombe hili.**

A. Aliyetenda, ukubwa, hali ya utendaji.
B. Aliyetenda, hali ya utendaji, ukubwa.
C. Mtendaji, aliyetenda, ukubwa.
D. Aliyetenda, ukubwa, hali ya mtendaji.

**18.** Kifaa kinachotumiwa kukatia nyasi huitwa

A. bero B. shepe
C. kwanja D. beleshi

**19.** $\frac{3}{5}$ kwa maneno ni

A. Thumni tano B. Humusi tatu
C. Thumni tatu D. Humusi tano

**20.** Ni sentensi ipi sahihi?

A. Ndizi lililoletwa ni langu.
B. Miti zilizopandwa zimeota.
C. Zulia iliyonunuliwa ni zuri.
D. Wema unaozungumziwa ni huu.

**21.** Chagua kinyume cha sentensi.

**Amani alisifiwa kwa utiifu wake.**

A. Amani hakusifiwa kwa utiifu wake.
B. Amani alikashifiwa kwa utundu wake.
C. Amani alikashifiwa kwa ukaidi wake.
D. Amani hakukaushifiwa kwa ukaidi wake.

**22.** Nomino **nyanja** imo katika ngeli gani?

A. U - ZI B. I - I
C. I - ZI D. LI - YA

**23.** Chagua jibu la kitendawili kifuatacho.

**Mimi nakula vyakula vyote vinono lakini sinenepi wala sikui.**

A. Ulimi na meno.
B. Chungu cha kupikia.
C. Mkono na vidole.
D. Kinu cha kusagia.

**24.** Eleza matumizi ya <u>kwa</u> katika sentensi.

**Mwalimu aliniita kwa kutaka kunikusoa.**

A. kwa ya mahali
B. kwa ya sababu
C. kwa ya pamoja
D. kwa ya kimilikishi

**25.** Taja tamathali ya usemi iliyotumika katika sentensi hii.

**Chakula cha shangazi kilikuwa asali.**

A. chuku B. sitiari
C. nahau D. tashbihi

**26.** Onyesha aina za maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi hii.

**Wanafunzi <u>hawa</u> ni <u>hodari</u> kuliko <u>wengine</u>.**

A. Nomino, kivumishi, kielezi.
B. Kivumishi, nomino, kiwakilishi.
C. Kivumishi, kivumishi, kiwakilishi.
D. Kiwakilishi, kivumishi, kivumishi.

**27.** Kamilisha methali:

**Kuku alaye mtama atakuwaje na ____?**

A. nyama B. mfupa
C. kidona D. manyoya

**28.** Ni jibu lipi lenye maelezo sahihi?

A. Sogora ni fundi wa kuimba na kukariri mashairi.
B. Mzegamzega huuza bidhaa rejareja.
C. Saisi hutunza wanyama wa uchukuzi.
D. Mjume ni fundi wa kufua visu.

**29.** Caro ameolewa na Jedi. Dada yake Caro ameolewa na Baraka. Baraka na Jedi wataitana

A. mwamu B. mwanyumba
C. kivyere D. shemeji

**30.** Shehena ni ya mizigo ilhali ________ ni la udongo.

A. tita B. peto
C. shumbi D. bumba

STEP FLYER SERIES

__*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 hadi 40.*__

Uamuzi uliofanywa na serikali wa kuhimiza watoto wote warudi shuleni ni jambo mwafaka. Watoto walifurika furifuri shuleni ili kusajiliwa. Wale waliokuwa wakirandaranda mitaani walifuatilizwa himahima na kupelekwa shule. Waliokuwa wakubwa ki-umri walipelekwa kwenye shule za ufundi. Wakatabasamu kwa furaha kama mzazi aliyepata salama.

Kwa miaka mingi **baadhi ya wazazi walikuwa wameshindwa kuwasomesha wana wao.** Hii ni kutokana na umaskini uliokithiri mipaka. Hali hiyo ilichangia huzuni kuu miongoni mwa familia. Pengo la waliosoma na wasiosoma lilizidi kuwa pana kielimu na kiuchumi. Uadui ukaingilia jamii. Ujambazi nao ukazidi.

Sasa watu wote wakipewa haki sawa ya kusoma hata wale watoto wa maskini watamanio masomo watakinaisha kiu yao. Pia mengi ya matatizo yatapungua. Si kweli kuwa tajiri ni mwerevu kuliko mkata. Kila mwanajamii akipewa nafasi na asome kwa bidii atafua dafu maishani.

Vijana watakaofuzu katika shule za kiufundi wataweza kuajiriwa katika sekta mbalimbali. Mwishowe wakipata mtaji watajiendeleza kwa kuanzisha miradi midogomidogo ya kujitegemea. Hali kama hii ikienea kote nchini viwanda vidogovidogo vitaanzishwa na ajira itapatikana. Hiyo itakuwa njia mojawapo kuu ya kuinua uchumi na kuzalisha nafasi nyingi za kazi. Kitaaluma, hawa vijana wataweza kuwa madaktari, wasanii, walimu.. na kazi zingine nyingi. Kisomo ni kitamu. Hakifai kutiliwa nanga.

---

**31.** Uamuzi uliofanywa na serikali
- A. ulisababisha kufurika kwa watoto shuleni na kupita mitihani.
- B. ulisababisha kuchipuka kwa vyuo vya ufundi na kuondoa umaskini.
- C. ulisababisha kuongezeka kwa watoto shuleni na kupata nafasi ya kujiendeleza
- D. ulisababisha kupungua kwa umaskini na kuwapa watoto nafasi ya kujiendeleza.

**32.** Kulingana na aya ya kwanza
- A. watoto walifurika furifuri shuleni kulipa karo
- B. wote waliingia shuleni na kusoma pamoja bila kuzingatia umri.
- C. waliokuwa wachanga ki-umri walienda shule za ufundi
- D. waliozidi umri wa kuingia shule za kawaida walipelekwa shule za ufundi.

**33.** ...baadhi ya wazazi walikuwa wameshindwa kuwasomesha wana wao. Chagua methali inayoweza kuelezea hali hii.
- A. Maskini halali mchana.
- B. Dua la mnyonge haliendi joshi.
- C. Maskini kupata ni mwenye nguvu kupenda
- D. Ng'ombe wa maskini hazai pacha.

**34.** Ni ukweli kuwa watu wote wakipewa nafasi sawa
- A. watoto wa maskini watakuwa werevu.
- B. watoto maskini na tajiri watakuwa sawa.
- C. watoto wote wapendao kusoma watakuwa matajiri.
- D. watoto wote wapendao kusoma watapata kisomo.

**35.** Maneno matatu miongoni mwa haya ni visawe vya neno maskini isipokuwa

A. fukara B. mlalaheri

C. mkata D. mlalahoi

**36.** Maana ya kusajiliwa ni

A. kurekebishwa

B. kunufaishwa

C. kuandikishwa

D. kufundishwa

**37.** Kisomo hakifai kutiliwa nanga kwa sababu

A. serikali itakigharamia

B. kina manufaa mengi

C. shule zitapanuka

D. watu watakuwa wataalamu

**38.** Ni sababu gani kuu inayowafanya vijana waliosomea kazi za ufundi wasifungue kazi zao za kujitegemea bali wao hutegemea kuajiriwa?

A. Kukosa maarifa ya kufanya kazi wenyewe.

B. Kukosa mtu wa kuwaelekeza ifaavyo.

C. Ukosefu wa mtaji.

D. Ukosefu wa miradi midogomidogo

**39.** Kulingana na kifungu, pengo kubwa la kiuchumi limesababishwa na ________

A. watoto kutopata kisomo kwa sababu ya umaskini.

B. uadui na ujambazi uliokumba jamii maskini

C. watoto kutopelekwa shule za ufundi kwa sababu ya umaskini

D. wazazi kushindwa kupambana na umaskini.

**40.** Kichwa kinachofaa zaidi kwa taarifa hii ni

A. Ukarimu wa serikali.

B. Kupunguza ujinga.

C. Masomo ya kifundi.

D. Serikali kupanua masomo.

STEP FLYER SERIES

***Soma kwa makini habari ifuatayo kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.***

Vijana ndio chumvi ya taifa. Wao ndio viongozi wa kesho. Wadau, wanataaluma na vinara wote wa kutegemewa wanatoka miongoni mwa vijana hawa. Taifa lisilo na vijana ni mfano wa gari bila mtambo au ujahazi bila tanga.

Ili taifa liwe bora la kutumaini, sharti vijana wake walelewe vyema, waelekezwe vizuri, wafunzwe adabu, nidhamu na maadili murua ili waje wawe waadilifu.

Katika kuwafunza na kuwaelekeza, vijana wahimizwe kusoma kwa bidii kwa juhudi na maarifa. Wawe wanyenyekevu na watiifu wa sheria za nchi na mataifa. Wawe na nidhamu mingoni mwao, wazee wao na watu wengine wa kila hirimu. Wasiwe washiriki wa ulevi wowote.

Vijana bora wenye nidhamu na wingi wa uadilifu hawarukii mambo ovyoovyo vururu mtende. Humakinika kwa kila walionalo na walisikialo. Hutenda baada ya kutafiti, kuchuja na kuchunguza. Naam, hapo ndipo hufanya na kufuata mambo yaliyo murua tu.

Ujana una vituko na vitimbi. Humfanya mwenye macho. Akawa hasikii ambapo anayo masikio yake mawili. Kumbuka kuharibika ujanani ni hasara na majuto ukubwani hasa uzeeni.

Tengeneza ujana wako leo ili unyooshe na kutakasa uzee wako kesho. Mustakabali wako au kesho yako ni muhimu kuliko leo yako ewe kijana. Sikia ujana ni kama moshi ukienda haurudi. Ama hujui hivyo?

**41.** Malezi mema kwa vijana ni

A. utajiri kwa taifa
B. tumaini kwa taifa bora la baadaye
C. kufunzwa ili waje wawe viongozi
D. kuwapeleka shuleni

**42.** Kwa nini vijana wamemithilishwa na chumvi ya taifa?

A. wao ni kiungo muhimu cha taifa.
B. wao ni wadogo au wachanga.
C. wao ndio tegemeo la kuleta maendeleo ya taifa.
D. Wao ndio wanaotumikia taifa.

**43.** Vijana bora ni

A. waliosoma sana hadi vyuo vikuu.
B. wanaoshikilia nyadhifa kubwa kubwa kazini.
C. wanaoshughulikia mambo ya kisasa kama vile, kucheza muziki na dawa za kulevya
D. wenye malezi mema, adabu, nidhamu na uadilifu.

**44.** Baadhi ya vituko vya ujana ni

A. michezo, riadha, masomo na muziki
B. ulevi, kiburi, ujeuri, uasi na kichwamaji
C. kusikia, kuona, kufuata na kushika
D. kuonea, kuzurura, kusaidia na kusoma.

**45.** Mambo yaliyo **murua** si pamoja na mambo

A. shambiro shambiro
B. aula uala
C. mufti mufti
D. aali aali

**46.** Watu wa kila hirimu ni

A. watoto wadogo
B. wazee wakongwe
C. watu wa makamo
D. wa umri wowote

**47.** Uadilifu wa vijana huwasaidia

A. kuyachunguza na kuyachuja mambo kabla ya kuyatenda
B. kusoma kwa bidii hadi ng'ambo
C. kuishi maisha ya kisasa na kushiriki raha leo
D. kuungana pamoja kuwapuuza wazee wao.

**48.** Taifa lisilo na vijana

A. ni kama gari au jahazi
B. halina uongozi bora
C. halina uhai
D. halitarajiwi kuendelea wala kupiga hatua kimaendeleo.

**49.** Mwisho mwisho tunaambiwa kwamba, maisha ya baadaye hasa uzeeni

A. yanaweza kutengenezwa kuwa mema kuanzia umri wa ujana
B. huharibikia uzeeni baada ya kutoka katika ujana
C. huwa mema baada ya kuharibikia ujanani.
D. yana umuhimu kuliko ya ujanani.

**50.** Chagua kichwa kisichofaa kuhusu habari hii

A. Ujana ni kama moshi.
B. Vijana ni tegemeo la taifa.
C. Vijana watakuwa sawa na wazee.
D. Ujana ni nguzo ya maisha.

STEP FLYER SERIES
STEP FLYER